# Nini kinaendelea kwenye shule zetu?

## Wananchi watafakari juu ya hali ya elimu Tanzania








## 1. Utangulizi

Tanzania imefanikiwa kupanua uandikishaji na upatikanaji wa elimu ya msingi: uwiano wa idadi ya watoto wenye umri wa miaka 7-13 wanaosoma shule za msingi ulikuwa asilimia 92 mwaka 2012 (Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi www.moe.go.tz). Wakati huo huo ishara nyingi zinaonesha kuwa kwenda shule siyo sawa na kujifunza. Ishara hizi zimetoka kwenye vyanzo vya Serikali, kwa mfano, kiwango cha kushindwa kwa wanafunzi wengi (61%) kwenye matokeo ya kidato cha nne ya mwaka 2012 yaliyojadiliwa sana (kukiwa na wanafunzi 6% tu waliopata daraja la I-III). Pia tathmini za ujuzi wa kusoma na kuhesabu Uwezo zinaonesha kuwa watoto wanashindwa kupata stadi muhimu za kusoma na kuhesabu wakiwa shule ya msingi (www.uwezo.net).

Matatizo haya yanaendelea kupanda hadi kwenye ngazi za juu za mfumo wa elimu zikifikia ngazi za chuo kikuu na hatimaye kudhihirisha mapungufu kwenye soko la ajira. Katibu Mtendaji wa Baraza la Vyuo Vikuu vya Afrika Mashariki (IUCEA) hivi karibuni alinukuliwa akisema "Vyuo vikuu kwenye Ukanda wa Afrika Mashariki vinazalisha nguvu kazi yenye nadharia tu, isiyo na ujuzi wala uwezo wa kiutendaji." Pamoja na mapungufu katika ngazi hizi zote haishangazi kuwa elimu imekuwa ni eneo la kipaumbele kwenye jitihada za Serikali.

Muhtasari huu unaripoti maoni ya wananchi ya hivi karibuni kuhusu shule zetu na ujifunzaji nchini Tanzania. Matokeo yametokana na awamu ya 17 ya *Sauti za Wananchi,* utafiti wa kwanza Afrika kwa njia ya simu za mkononi wenye uwakilishi wa kitaifa (www.twaweza.org/sauti). Takwimu zilikusanywa kutoka kundi la wahojiwa wanaotoka maeneo yote Tanzania Bara. Simu zilipigwa kati ya Aprili 22 na Mei 20, 2014; matokeo haya ni majibu kutoka kaya 1,442.

Muhtasari huu umeandikwa na kuchapishwa na Twaweza, iliyopo Hivos Tanzania. Wachangiaji ni Youdi Schipper, Elvis Mushi, Risha Chande na Rakesh Rajani. Takwimu zilikusanywa na Ipsos Tanzania. Umetolewa mwezi Julai 2014

S.L.P 38342, Dar es Salaam, Tanzania.
Simu: +255 22 266 4301 | barua pepe: uwazi@twaweza.org
www.twaweza.org/sauti

Matokeo muhimu ya muhtasari huu ni:

- Asilimia 91 ya wanafunzi wanakaa kwenye fomu au dawati wakiwa darasani, lakini ni asilimia 49 tu ndiyo wanaopata chakula shuleni
- Asilimia 69 ya wanafunzi wanaripoti kuwa ni "nadra sana" au "hawapewi kabisa" kazi za masomo za kufanyia nyumbani
- Wanafunzi wa shule ya msingi walioko kwenye asilimia 38 ya kaya wanaripoti kuwa mwalimu wao hakuingia darasani siku nzima siku moja kabla ya mahojiano
- Asilimia 35 ya wananchi wanakadiria kuwa wanafunzi chini ya asilimia 25 ndiyo wanaokuwa wamepata ujuzi wa ngazi ya darasa la 2 baada ya kumaliza darasa la 2.
- Licha ya kuwa na viwango duni vya kujifunza ni vigumu kukuta mtoto yeyote ameacha shule kwa sababu ya utendaji duni wa kimasomo.
- Asilimia 15 ya wananchi wanafahamu mpango wa Matokeo Makubwa Sasa.

# 2. Mambo nane kuhusu elimu nchini Tanzania

## Jambo la 1: Takwimu za msingi

**Katika 86% ya kaya ya Tanzania angalau mtoto mmoja anasoma shule ya msingi.**

**Katika 95% ya kaya ya Tanzania angalau mtoto mmoja anasoma shule ya msingi ya Serikali.**


**Chanzo cha takwimu:** Utafiti wa *Sauti za Wananchi* – Awamu ya 17, Aprili-Mei 2014.

Ukijumlisha kaya zote, mwaka 2012 takriban watoto milioni nane walikuwa wanasoma shule za msingi za Serikali nchini Tanzania (Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, www.moe.go.tz).

## Jambo la 2: Karibu wanafunzi wote hukaa kwenye madawati

Kielelezo cha 1 kinaonesha takwimu kuhusu hali ya shule zilizopatikana kutokana na mahojiano na wanafunzi wa shule ya msingi. Wanafunzi hawa walisema kuwa karibu kila siku wanapofundishwa darasani, mara nyingi hufundishwa na mwalimu wa kiume (76%), na huwa wamekaa kwenye fomu au dawati (91%). Hata hivyo, mara nyingi wanafunzi (51%) hawana kitu chochote cha kula wakati wakiwa shuleni.

**Kielelezo cha 1: Hali ya Shule – mahojiano na wanafunzi**





**Chanzo cha takwimu:** Utafiti wa *Sauti za Wananchi* – Awamu ya 17, Aprili-Mei 2014.

## Jambo la 3: Walimu mara nyingi hawako darasani

Wanafunzi wa shule ya msingi ambao walihudhuria shule siku moja kabla ya mahojiano waliulizwa kuhusu mahudhurio ya mwalimu wao. Matokeo (Kielelezo cha 2) yanaonesha kuwa asilimia 34 ya walimu walikuwa darasani, wakati asilimia 38 ya walimu hawakuwa darasani wakati wote. Hii ina maana kuwa, ni walimu 3 tu kati ya 10 ndiyo wanaoingia darasani muda wa vipindi vya masomo.

**Kielelezo cha 2: Je, mwalimu wako aliingia darasani jana?**





**Chanzo cha takwimu:** Utafiti wa *Sauti za Wananchi* – Awamu ya 17, Aprili-Mei 2014.

## Jambo la 4: Kazi za masomo kufanyika nyumbani ni nadra shule za msingi

Wanafunzi saba kati ya kumi walisema kuwa ni "mara chache" au "hawapewi kabisa" kazi za masomo za kufanya nyumbani (kumbuka kuwa wanafunzi walichaguliwa kutoka madarasa yote katika shule ya msingi). Wale ambao hupewa kazi za masomo za kufanyia

nyumbani hawapati msaada kwenye kazi hizo. Hata hivyo, kwenye maeneo mengi kazi za masomo za nyumbani husahihishwa (64%) na / au kupitiwa na wazazi (68%) "mara kwa mara" au "kila siku".

**Kielelezo cha 3: Kazi za masomo kufanyia nyumbani**





**Chanzo cha takwimu:** Utafiti wa *Sauti za Wananchi* – Awamu ya 17, Aprili-Mei 2014.

## Jambo la 5: Familia nyingi hupokea ripoti za maendeleo ya wanafunzi

Wazazi wa wanafunzi wa shule za msingi wanaonyesha kuwa shule zao hutoa taarifa za maendeleo ya wanafunzi kwa wazazi: hata hivyo familia moja kati ya tano haikupokea taarifa ya maendeleo ya wanafunzi ndani ya miezi sita iliyopita.

**Kielelezo cha 4: Je, familia yako ilipokea taarifa ya maendeleo ya mwanafunzi ndani ya miezi sita iliyopita?**





**Chanzo cha takwimu:** Utafiti wa *Sauti za Wananchi* – Awamu ya 17, Aprili-Mei 2014.

## Jambo la 6: Kufukuzwa kwa wanafunzi wa shule ya msingi ni kitu nadra sana

Baadhi ya wazazi (6%) wenye watoto wanaokwenda shule walisema kuwa mtoto mmoja kati ya walionao aliacha shule akiwa shule ya msingi mwaka jana. Sababu za kukatisha masomo zilitajwa kuwa mara nyingi "wanafunzi hawakuvutiwa na mazingira ya shule" na wengine walisema "shule ziko mbali sana kutoka nyumbani" na "hawana fedha ya ada, sare za shule, vitabu".

**Kielelezo cha 5: Je, kaya yako ina mtoto mwenye umri wa miaka 6-16 ambaye ameacha shule katika kipindi cha mwaka jana?**




**Chanzo cha takwimu:** Utafiti wa *Sauti za Wananchi* – Awamu ya 17, Aprili-Mei 2014.

Kaya chache sana zilitaja kushindwa mitihani kama moja ya sababu ya wanafunzi kuacha shule (asilimia 3.5 ya kaya ambazo mtoto aliacha shule). Hii ni jambo la kawaida maana watoto wengi wana utendaji ulio chini ya viwango rasmi vya mtaala. Kwa mujibu wa utafiti wa Uwezo, asilimia 57 tu ya watoto wa darasa la 3 au madarasa ya juu walikuwa na uwezo wa kusoma hadithi rahisi ya darasa la 2 kwa Kiswahili mwaka 2012. Hii ina maana kuwa wanafunzi wengi hufika madarasa ya juu ya shule za msingi bila kuwa na ujuzi wa kusoma kwenye ngazi ya darasa la 2.


## Jambo la 7: Wananchi wengi wana matarajio madogo (na sahihi) kuhusu viwango vya kujifunza

Je, wananchi wanasemaje kuhusu uwezo wa wanafunzi wa darasa la 2? Ni asilimia ngapi ya wanafunzi wanaodhani kuwa wanaweza kusoma na kuhesabu katika ngazi ya darasa la pili ? Na ni asilimia ngapi inayodhani inapaswa kuwa na uwezo wa kusoma na kuhesabu?

Kielelezo cha 6 kinaonesha kuwa wananchi hawana matumaini juu ya uwezo halisi wa kujifunza kwa watoto: wengi (35%) wanaamini kuwa wanafunzi chini ya 25% ndiyo wanaokuwa na ujuzi wa kusoma na kuhesabu kwa kiwango sahihi ifikapo mwisho wa darasa la 2 (kinyume na wananchi 10% wanaoamini kuwa zaidi ya 75% ya wanafunzi huwa tayari

wana ujuzi wa kusoma na kuhesabu). Matokeo ya tathmini kubwa ya ujifunzaji inayofanywa na Uwezo yanaonesha kuwa ni mtoto 1 tu kati ya 5 wa darasa la 3 anayeweza kufanya hesabu za kuzidisha na kusoma hadithi rahisi ya Kiswahili[1] - hii ina maanisha, wananchi idadi kubwa wana taarifa za kutosha lakini wengi hawana matumaini makubwa. Kielelezo cha 6 pia kinaonesha kuwa ni asilimia 31 tu ndio wanasema kuwa wanafunzi zaidi ya 75% wanapaswa kuwa na ujuzi wa kiwango cha madarasa yao, kiionyesha kuwa matarajio ya mfumo wa elimu yako chini.

**Kielelezo cha 6: Unapofikiri juu ya watoto wote wa Tanzania ambao hivi karibuni wamemaliza darasa la 2, unadhani ni asilimia ngapi wanaweza kusoma na kuelewa hadithi ya darasa la 2 na kufanya hesabu za darasa la 2? Na ni asilimia ngapi wanaopaswa kuweza kufanya hivyo?**





**Chanzo cha takwimu:** Utafiti wa *Sauti za Wananchi* – Awamu ya 17, Aprili-Mei 2014.

## Jambo la 8: Wananchi asilimia 16 wanafahamu Mpango wa Matokeo Makubwa Sasa

Katika jitihada za kuifanya nchi kuwa yenye uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025, na kupata msukumo kutoka kwenye uzoefu wa nchi ya Malaysia, Tanzania ilipitisha mpango wa Matokeo Makubwa Sasa (*Big Results Now,* BRN) mwaka 2013. Mpango huu unalenga kufikia matokeo yanayohitajika kwenye sekta kadhaa muhimu, ikiwa ni pamoja na elimu, maji na kilimo. Kwa mujibu wa taarifa zilizopo kwenye tovuti ya Ofisi ya Waziri Mkuu - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, "...umma utashirikishwa kujifunza kuhusu mipango ya maendeleo na kushirikishana maoni yao ipasavyo." Kwa mujibu wa takwimu za *Sauti za Wananchi* ni Watanzania wachache tu (16%) ndiyo wenye ufahamu wa mpango wa Matokeo Makubwa Sasa.

1 Angalia http://www.uwezo.net/publications/reports/ kwa taarifa za kina na ripoti.

**Kielelezo cha 7: Je, unafahamu kuwa mapema mwaka jana Serikali ya Tanzania ilizindua mpango mpya wa Matokeo Makubwa Sasa (BRN)?**




**Chanzo cha takwimu:** Utafiti wa *Sauti za Wananchi* – Awamu ya 17, Aprili-Mei 2014.

Wale wanaoufahamu Mpango wa Matokeo Makubwa Sasa mara nyingi wametaja elimu kama sekta mojawapo ambayo mpango huu unatekelezwa. Walipoulizwa kama wameona mabadiliko yenye mafanikio yoyote, wananchi asilimia 6 tu ndio waliosema ndiyo (asilimia 36 ya wale wanaoufahamu wa mpango). Kati ya mabadiliko hayo, baadhi wametaja maboresho kama “walimu wameongezwa” na “watoto wanapewa elimu bora”.

## 3. Hitimisho

Muhtasari huu unatoa dondoo za ukweli muhimu na maoni ya wananchi kuhusu ujifunzaji kwenye shule za msingi nchini Tanzania, ambayo ni msingi wa mfumo wa elimu. Mambo haya mengi yanatia wasiwasi. Familia nchini Tanzania kwa kawaida zina mtoto mmoja au zaidi anayesoma shule ya msingi. Wafikapo shuleni, watoto hawa hukaa darasani lakini mara nyingi huwa hawana mwalimu; na ni mara chache watoto hawa hupatiwa kazi za masomo kufanyia nyumbani. Hata hivyo, wazazi hupokea taarifa ya maendeleo ya mtoto wao.

Wazazi wengi wanatambua kwa usahihi kabisa kuwa viwango vya kujifunza viko chini lakini wengi wao *hawadai maboresho ya matokeo ya kujifunza yanayotakiwa.* Juhudi ndogo za kudai ubora ni kitu kinachotia wasiwasi kwa mamlaka za elimu za taifa na wananchi pia: kama wazazi wana matarajio na shauku na madai madogo kiasi hicho, kuna mtu yeyote atayekuwa na motisha ya kufuatilia matokeo ya kujifunza kwenye ngazi za chini – ambako ni muhimu zaidi? Utafiti-fuatilizi unatakiwa uulize; inawezekanaje wazazi wana shauku ndogo kiasi hicho ya kudai ubora wa elimu: ina maana hawaoni thamani ya ujuzi wanaojifunza watoto? Je, wahusika wengine, kama vile wakaguzi wa shule, wanaweza kudhibiti ubora kwa ufanisi katika ngazi ya shule?

Kuna tatizo linalohusiana na hayo kwenye shule za msingi Tanzania: tangu mwaka 2009, wanafunzi wanaofanya vibaya kwenye masomo wanaruhusiwa kuendelea madarasa ya juu lakini wanatakiwa kuhudhuria vipindi vya masomo ya kujirekebisha[2]. Hii inasababisha tatizo la msingi la kimotisha, kwa sababu walimu sasa hawawezi kutimiza wajibu wao muhimu wa kuhakiki ubora kwa kufundisha watoto kulingana na uwezo wao.

Kutojali tofauti za msingi za mwanafunzi ndani ya madarasa kunaweza kupoteza motisha ya kusisitiza ubora shuleni. Hakuna hatua kwa mwanafunzi iwapo akishindwa kufikia viwango vya uwezo vinavyotakiwa kwa sababu kupandishwa darasa na wanafunzi wenzake wenye uwezo ni suala la uhakika. Kwa walimu, mfumo unaashiria kutokuwa na shauku ya kujikita kwenye ubora na ujifunzaji unaomlenga mtoto. Hii inatia wasiwasi, kwa maana kuna ushahidi kutoka tafiti Afrika ya Mashariki kuwa kutofautisha kati ya wanafunzi wenye uwezo wa juu na wale wenye uwezo wa chini, kunaweza kuleta tofauti kubwa kwenye maendeleo ya ujifunzaji kwa wanafunzi wote wenye uwezo wa chini na wale wenye uwezo wa juu[3]. Hii pia ina athari kwenye motisha ya mwalimu, kama inavyothibitishwa na uwepo wa viwango vya juu ya utoro ulioripotiwa kupitia utafiti wa *Sauti za Wananchi.*

Serikali ya Tanzania imeamua kukabiliana na changamoto ya kuboresha matokeo ya kujifunza kwenye shule zake za msingi. Hatua zimechukuliwa kuboresha upatikanaji wa vitabu vya kiada na kufuatilia upokeaji ruzuku ya uendeshaji kwa ajili ya kugharamia vifaa vya kujifunzia. Mpango wa Matokeo Makubwa Sasa (BRN) unalenga kuboresha matokeo ya kujifunza. Hata hivyo, tunajuaje kipi kinaleta manufaa kwenye kuboresha elimu?

Hatua kwenye sekta ya elimu zote kwa pamoja zinashindania rasilimali chache: kila shilingi inaweza hutumiwa mara moja tu. Hivyo, ni muhimu kuwa hatua zilete manufaa ya kuboresha matokeo ya kujifunza. Bila hili, hakuna uhakika kuwa thamani ya fedha inapatikana. Kwa maneno mengine, watunga sera wanapaswa kutumia ushahidi kuwashawishi walipa kodi, wadau wa elimu na wanasiasa kuwa fedha za kodi zinatumika kwenye sera zinazoleta manufaa na ambazo "zinanunua" matokeo ya kujifunza. Vivyo hivyo, sera ambazo hazioneshi kuleta manufaa hazistahili kupatiwa fedha hizi chache za walipa kodi. Aina hii makini ya matumizi ya fedha inahitaji ushirikiano wa watunga sera, wana sayansi na wanasiasa kufikiri na kutenda pamoja kwa kutumia ushahidi kuboresha elimu.

2 UNESCO, Uchambuzi wa Sekta ya Elimu Tanzania, 2011.

3 Angalia kwa mfano Duflo, E., Dupas, P., & Kremer, M. (2011). kuathiriana kwa rika, motisha mwalimu, na athari za kufuatilia: Ushahidi kutoka tathmini ya uchunguzi nchini Kenya. Mapitio ya Uchumi wa Amerika, 101, 1739-1774